**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Ruzinga

S.L.P 1895

**BUKOBA**.

MEI, 2024.

**Namba za simu**:
Mkuu wa shule – 0758029457
Makamu Mkuu waShule - 0757928419
Mwl Mlezi 0765262753

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi…………………………..
S.L.P …………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUZINGA HALMASHAURI YA MISSENYI MKOA KAGERA MWAKA 2023**

1.0. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2023/24 tahasusi ya PCB .Shule ya Sekondari Ruzinga iliyopo umbali wa kilometa 60 kutoka makao makuu ya Wilaya. Shule ipo kata Ruzinga iko kilometa 52 kaskazini magharibi mwa mji wa Buboba. Usafiri upo ukiwa unatoka Mji wa Bukoba utapanda gari nauli sh 4000/= kutoka Bukoba mjini hadi Ruzinga Sekondari,

Muhula wa masomo unaanza tarehe 1/07/2024. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 29/6/2024 mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/7/2024

## 2.0Mambo muhimu ya kuzingatia

### 2.1. Sare ya shule (Uniform).

(i)Shati nyeupe 2 **aina ya tomato**zenye mikono mirefu na zisizo na urembo wowote.

(ii)Soksi nyeupe jozi 2 (**siyo stocking**).

(iii) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi, vyenye kufunika miguu na visivyo na urembo wowote, jozi 2.(**Siyo mfano wa buti**)

(iv) Nguo za michezo ambazo ni "track suit" ya bluu bahari kitambaa kizito kisichoteleza, isiyo bana na isiyo na kofia (**Adidas**) na raba nyeupe (**Siyo mfano wa buti**), jozi moja.

(v) Sweta rangi ya kijivu shingo ya "V" yenye michirizi ya blue bahari miwili shingoni, mikononi nakiunoni ikiwa na nembo ya shule upande wa kushoto.

(vi) Tai yenye michirizi ya rangi nyeupe na blue bahari na nembo ya shule.

(vii) Sketi blue bahari mbili (2), kitambaa kizito (Esteem) yenye mshono wa "linda box ya malinda michirizi miwili ya kitambaa cheupe cha tetron inalala mbele kwenye linda la mbele) Sketi iwe ndefu hadi miguuni.

(viii) Nguo za nje ya darasa (shamba dress) Gauni 2 rangi ya zambarau kitambaa cha tetron nzito au Esteem na siyo aina nyingine ya kitambaa. Mshono wa soro na shingo ya duara, Gauni iwe ndefu hadi miguuni.

(ix) "T- Shirt" moja rangi ya kijivu yenye kola isiwe na mwandishi Wala alama yoyote (**form six**) kitambaa kizito yenye nembo ya shule upande wa kushoto na nyuma mgongoni.

**TANIBIHI: Mwanafunzi aje amevaa gauni ya zambarau sare ya shule tajwa hapo juu, asije na nguo yoyote ya nyumbani.**

**ANGALIZO**

Kuepuka usumbufu, utata wa rangi na mishono yaa sare za shule,sare hizo zinapatikana maeneo ya shule kwa gharama ifuatayo; sweta yenye nembo ya shule Tsh 15000/=,T-shirt ya kijivu yenye kora na nembo ya shule Tsh 15000/= na, Tai nyenye nembo michirizi mieupe na blue bahari Tsh 5000/=

**Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

(i) Madaftari makubwa yasiyopungua 10 (counter books)
(ii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
(iii) Rula, kalamu za wino na pencil za kutosha muhula
(iv) Dictionary
(v) Karatasi (Photocopy papers-double A) Ream 2 kwa mwaka.
(vi) Scientific Calculator (wanafunzi wa sayansi)
(vii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
(viii) Stop watch(digital)
(ix) Mto mmoja (1) na foronya mbili (2) za rangi ya pinki.
(x) Mashuka manne (4 ) ya pinki yasiyo na maua na blanketi moja (1).
(xi) Graph pad kubwa yenye kurasa 50 hii ni kwa wanafunzi wa sayansi tu.
(xii) Godoro moja (1) la futi 2½ na chandarua kimoja (1)
(xiii) Nguo ya kulalia(**night dress**)
(xiv) Jozi moja (1) ya kanga/vitenge.
(xv) Sahani 1, bakuli 1, kikombe 1, kijiko 1, vyombo vyote viwe vya bati au plastiki.
(xiv) Toilet papers (karatasi za chooni) kumi (10).

(xv) Kifaa cha maji ya kunywa kidumu cha lita tano.
(xvi) Taulo moja (1).
(xvii) Nguo za ndani (gagulo (underskirt) 2, chupi zisizopungua 6 na sidiria 3).
(xviii) Vifaa maalum vya matumizi ya msichana, Always paketi 4).
(xix) Sabuni, mswaki, dawa ya meno,mafuta ya kujipaka, dawa ya viatu.
(xx) Jembe1, mifagio ya ndani na nje 1, brashi kwa ajili ya usafi wa vyoo na bafu (Squeezer/Fraps 1 & hard brush 1)
(xxi) Ndoo ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 20 na beseni moja la kuogea
(xxii) Box file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake za mitihani (mali ya mwanafunzi) spring file moja la kutunza taarifa zake ofisini.
(xxiii) Aje na Bima ya Afya ya mwanafunzi inayotolewa na (NHIF)
(xxiv) Fedha za matumizi binafsi. Shule hutoa chakula, mpatie binti yako fedha kidogo kwa ajili ya matumzi yake ya kawaida awapo shuleni. Fedha nyingi humfanya ashindwe kufuata masomo ipasavyo.

Michango mbalimbali

1.Tahadhari 5000/=

2.Nembo kwaajili ya kuweka kwenye mashati 5000/=

3.kitambulisho cha shule 5000/=

4.Michango ya uendeshaji wa shule 65000

JUMLA=80000/=

Fedha taslimu zote zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na 32601100025 benki ya NMB yenye jina RUZINGA SEKONDARI RECCURENT ACCOUNT.(Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye slipu na kuja nayo shuleni.)

## 3.0. Viambatisho na fomu muhimu

Binti yako atatakiwa kukamilisha na kuleta viambatisho au fomu kama ifuatavyo:

(a) **Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form**)
Ni lazima binti yako apimwe katika Hospitali ya Serikali na daktari anayehusika kukamilisha vipengele vya afya yake . Fomu hii ni lazima iwasilishwe shuleni mara anaporipoti.

(b) **Nakala ya cheti cha Uraia -** Alete nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) au cheti cha utambulisho wa uraia, ambacho hupatikana kwa Mkuu wa Wilaya yako. Kumbuka hatutakubali utambulisho wa kijiji, Kata au Tarafa.

(c) **Taarifa Binafsi -** Fomu maalum imeambatanishwa, fomu hii ijazwe kwa uangalifu na kurudishwa hapa shuleni anapokuja kuripoti.

(d) **Picha za utambulisho wa wazazi na walezi -** Weka picha za hivi karibuni kwenye chumba husika kama ilivyo kwenye taarifa binafsi kipegele B, C na D. Hatasikilizwa mzazi au mlezi kwa shauri lolote linalohusu mwanafunzi iwapo taarifa binafsi hazitajazwa kwa ukamilifu na kuweka picha.

(e) Picha moja(1) ya mwanafunzi (passport size ibandikwe kwenye form yake ukurasa wa mbele

**N.B. Mwanafunzi alete hati ya matokeo (result slip) yake ya kidato cha nne akiwa ametoa 'copy'**

## 4.0. Mambo mengine muhimu ya kuzingatia:

Kuna likizo fupi mbili kwa mwaka na likizo mbili ndefu kwa mwaka. Wakati huu shule huruhusu wanafunzi wote kwenda nyumbani hivyo kila mzazi anawajibika kusafirisha mtoto wake. Shule huwaruhusu

vijana wote ili wasafiri kwenda kwa wazazi/walezi wao na siyo kwingineko. Ni jukumu la mzazi kuhakikisha ya kuwa umempokea mtoto wako na kumtunza inavyopaswa. Ni mategemeo ya shule kuwa wakati huu vijana watatumia muda wao vizuri kwa kuwasaidia wazazi kufanya shughuli mbalimbali za kuzalisha mali na kusoma, badala ya kuzurura ovyo.

Ni sheria ya shule kwamba baada ya likizo kila mzazi ahakikishe mtoto wake anawahi shuleni katika siku na tarehe zilivyopangwa na analeta mahitaji yote muhimu. Akichelewa aje na mzazi /mlezi la sivyo atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**5.0 Mwisho**:

Hakikisha umekamilisha mahitaji yote na kujaza fomu zote kabla ya kumleta mtoto shuleni. Cheti cha uraia, fomu ya taarifa binafsi na Fomu ya Afya na sheria za shule zilizotiwa sahihi lazima virudishwe shuleni.

Angalizo: Mwanafunzi atakayepatikana kufanya udanganyifu katika ujazaji wa fomu ya afya hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Kwa niaba ya jumuiya nzima ya Shule ya Sekondari Ruzinga napenda kumpa hongera binti yako kwa kushinda mtihani na kuchaguliwa kujiunga na shule hii. Tunauhakika akifuata sheria za shule na akasoma kwa bidii na kwa malengo atafanikiwa.

**KARIBU SANA**

**MATINDE C. EMMANUEL**
**MKUU WA SHULE**

## 6.0 SHERIA ZA SHULE

**JINA LA MWANAFUNZI ____________________________ KIDATO CHA ____ MWAKA ____**

**(a) Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule**:

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa au utoro.

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu au walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi ulikubalika na uongozi wa shule.

(vii) Ulevi wa kunywa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

(viii) Kudharau Bendera ya Taifa.

(ix) Uvutaji bangi/sigara.

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja na kuolewa.

(xi) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu au laini ya simu ya mkononi katika kazingira ya shule.

(xii) Kupata ujauzito au kutoa mimba.

(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xiv) Kufanya jaribio lolote kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xv) Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xvi) Uaribifu wa mali ya umma kwa makusudi

(b) **Mwanafunzi awapo shuleni hapaswi kufanya yafuatayo**:

- Kufuga kucha ndefu

- Kupaka rangi kwenye kucha, mdomo, kope au nyusi
- Kutumia vipodozi
- Kukata nywele kwa mitindo iliyo tofauti na maelekezo ya Mwandamizi wa Malezi na nidhamu
- Kuvaa nguo fupi au zinazobana mwili.
- Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kumiliki simu ya mkononi,line ya simu,earphone,charger,power bank,pasi ya umeme na redio

(c) **Mwanao awapo shuleni atatakiwa**.

(i) Kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa.
(ii) Kuvaa sare ya shule /ya kazi wakati wote (kulingana na maelekezo atakayopewa)
(iii) Kutii amri .na sheria zote za shule
(iv) Kujiheshimu, kuheshimu wenzake, viongozi, walimu na watu wote kwa ujumla.
(v) Kutunza mali zake na mali za umma.

(d) **Heshima**

(i) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuamkia walimu, wafanyakazi wasio walimu pia mtu/mgeni yeyote anayemzidi umri anapopita na anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
(ii) Mwanafunzi kama kila raia mwema, lazima aheshimu Bendera ya nchi yake na wimbo wa Taifa.
(iii) Matusi, lugha chafu na kupigana ni dalili ya kukosa nidhamu.

(e) **Utii**

(i) Kila mwanafunzi hana budi kutii na kufuata maelekezo na maagizo ya viongozi wa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wasio walimu.

(ii) Mwanafunzi anapoitwa mahali lazima aitike, na kukimbia kule aliko kiongozi anayemuita (iii) Kiburi, majibu ya jeuri na matumizi ya lugha mbaya haviruhusiwi.

(iv) Ni wajibu kila mwanafunzi kufanya na kukamilisha kazi anayopangiwa iwe nje au ndani ya darasa

(f) **Upendo**

Mwanafunzi ajipende yeye mwenyewe, na awapende wenzake kama ndugu zake wa shuleni, awapende walimu kama walezi wake, aipende shule yake kama nyumbani kwake, aipende na kujivunia nchi yake ya Tanzania.

(g) **Ruhusa**

Ruhusa maalum ya kutoka nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule tu kwa sababu maalum

(h) **Mambo ya msiba**

Mwanafunzi akifiwa akiwa shuleni ataruhusiwa kuomboleza shuleni tu. Taarifa zote za kifo zitapashwa zipitie kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule. Ruhusa ya kwenda nyumbani itatolewa na Mkuu wa Shule endapo mwanafunzi atakuwa amefiwa na baba/mama mzazi au ndugu yake wa baba na mama.

(i) **Mabadiliko ya anwani**

Unashauriwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Shule iwapo anwani inayotumika kwa mawasilino imebadilika.

(j) **Ripoti**

Shule hutuma taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia na kitaaluma kila muhula. Tafadhali hakikisha unaipata, na kutuma maoni yako shuleni.

JE UNAKUBALI? **NDIYO**☐**HAPANA**☐
(Weka alama ya √ panapohusika)

Jina la Mwanafunzi_____________________ Sahihi _______ Tarehe ____________

Jina la Mzazi ________________ _________ Sahihi _______ Tarehe ___________

ANUANI ..............................

............................................

............................................

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Ruzinga,
S.L.P. 1895,
**BUKOBA.**

**TAARIFA BINAFSI**

A. Jina la Mwanafunzi
.................................................................................................

Anwani ya nyumbani
................................................................................................ ..

.................................................................................................................................

Kabila ........................................ Tarehe ya kuzaliwa
............./..................../20.....................

Mtanzania /Si Mtanzania

Dini ya Mwanafunzi....................... Mtaa/Kijiji …………. Jina la mratibu elimu kata/mtendaji

…………………namba za simu……..…………......Wilaya....................Mkoa..............................

B. Jina la Baba ................................................ * (Hai/Marehemu) ................................

(Mwaka aliofariki)

.............................

Dini ya Baba ................................. Kazi ya Baba ............................... Simu Na ....................

Jina la Mama ................................................ *(Hai/Marehemu) ....................................

(Mwaka aliofariki).................................

Dini ya Mama .............................. ................ Kazi ................................. Simu Na. ................

C. Taja majina na anuani za Walezi/Ndugu wengine wawili wasiokuwa wazazi wanaoruhusiwa kufika shuleni kusikiliza matatizo ya mtoto na kutoa maamuzi juu ya mashauri ya mtoto wako.

JINA.................................................. Uhusiano ......................umri……...SIMU NA. .....................

JINA ............................................. Uhusiano.......................umri……...SIMU NA …………

**B.picha za wazazi**

| | |
|---|---|
| | |

**C.picha za walezi**

| | |
|---|---|
| | |

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**

**FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION**

Student's Name ………………………………………………………………………………………………..

Blood Examination: Haemoglobin …………………………Blood Group ……………………………………..

Stool Examination ………………………………………………………………………………………………...

Urinalysis
…………………………………………………………………………………………………

Pregnancy
test…………………………………………………………………………………………………..

T.B. Test (If negative, was immunization
given)……………………………………………………………..

Eyes…………………………………………………………………………………………………
…………

Chest
…………………………………………………………………………………………………
……

Any chronic complaints not noted above e.g.

Asthma
…………………………………………………………………………………………………
…

Headache
…………………………………………………………………………………………………

Inability to eat certain foods …………………………… Skin

diseases etc…………………

Also anything that the School health staff should know
about…………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………………
…………..

Any treatment given or recommended
…………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………
…………..

**NOTES**: If any of the examinations requested above cannot be carried out, it is useful if it is noted that they have not been done rather than writing NAD down. In case of Bilharzia it is recommended that students attend the Bilharzia clinic before they come to school.

Signature of Examiner ……………………….

Designation …………………………………..

Date……………………………………………